

# MJADALA WA KIITIKADI

حوار عقائدي

**Mtungaji:**

Fadhil Muhammad

**Mtarjumi:**

Abdul Karim Juma Nkusui

**Kimepitiwa na:**

Mubarak A. Nkanatila

ترجمة

حوار عقائدي

تأليف

فاضل محمد

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:  
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 – 17 – 064 – 7**

**Mtungaji:**

Fadhil Muhammad

**Mtarjumi:**

Abdul Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**

Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimepitiwa na:**

Mubarak A. Nkanatila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**

Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza: Mei, 2014**

Nakala: 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

Alitrah Foundation

S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555

**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com

**Tovuti:** www.ibn-tv-com

**Katika mtandao:** www.alitrah.info



---

---

## YALIYOMO

---

Neno la Mchapishaji .....	1
1 - Kutawasul kwa Mawalii na watu wema .....	5
2 - Kuapa kwao, kuzuru makaburi yao na kuweka nadhiri kwao .....	12
3 - Kujengea makaburi na kuyapamba.....	17
4 - Majina ya kuungwa .....	19
5 - Kusujudu juu ya turba.....	20
6 - Kubusu dharihi .....	22
7 - Masahaba wangu ni kama nyota.....	25
8 - Shahada ya tatu .....	26
9 - Kukusanya baina ya Swala mbili.....	28
10 - Taqiyya .....	31
11 - Umaasumu .....	34
12 - Kupotoshwa kwa Qur'ani.....	36
13 - Uadilifu wa masahaba .....	39
14 - Muta'a.....	44
15 - Ukhalifa .....	46



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

---

## NENO LA MCHAPISHAJI

---

**K**itabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *Hawaaru 'Aqa'idi*. Sisi tumekiita, *Mjadala wa Kiitikadi*. Kitabu hiki kimeandikwa na Fadhil Muhammad.

Maudhui ya kitabu hiki ni kuhusu baadhi ya masuala ya kiitikadi na kuhitilafiana kwa madhehebu kuhusiana na itikadi hizo. Mwandishi wa kitabu hiki anatuletea mjadala kuhusu maudhui zifuatazo:

- Tawasuli kwa mawalii na watu wema
- Kuapa kwao, kuzuru makaburi yao na kuweka nadhiri kwao
- Kukusanya kati ya swala mbili
- Uadilifu wa masahaba
- Majina yaliyoungwa
- Kujengea makaburi na kuyapamba

Kwa bahati mbaya sana, kuna baadhi ya Waislamu wanawakufurisha Waislamu wenzao kwa kuwa tu wanaamini juu ya masuala hayo hapo juu na kuyatekeleza vilivyo. Watu hao wanawatuhumu wenzao bila dalili. Mwandishi wa kitabu hiki anajaribu kuondoa utata huu kwa ufafanuzi wa kielimu na dalili kutoka katika Qur'ani Tukufu na Sunna na pia katika historia.

Msomaji wetu utakaposoma kwa makini na bila chuki yoyote na mawazo pandikizi utagundua ukweli wa mambo haya kwamba ni yenye asili katika dini.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa makubwa hususan wakati huu wa sayansi na teknolojia kubwa ambapo ngano, hadithi za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi kwa watu wa sasa.

Taasisi yetu ya Al-Itrah imeona ikichapishe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa makubwa kwao.

Tunamshukuru Ndugu yetu Ustadh Abdul Karim J. Nkkusui kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah Mwenyezi Mungu 'Azza wa Jallah amlipe kila la kheri hapa duniani na huko Akhera pia; bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah Mwenye kujazi awalipe wote malipo mema duniani na Akhera pia.

**Mchapishaji:**  
**Al-Itrah Foundation**



## بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

### **KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU**

**I**likuwa ni asubuhi inayoburudisha macho na inayofurahisha nyoyo kwa utulivu wake, nilianza kutaamali katika uzuri wake na uzuri wa mandhari yake ambayo tunayapita kwa mabasi makubwa na mazuri, watengenezaji wake wameyaunda vizuri na yanadhihirisha teknolojia ya kisasa yenye kuvutia, kando yangu alikuwepo mwanaume mzuri aliyevalia mavazi yenye kupendeza pamoja na miwani mizuri akanianza kwa kusema: “Unaonaje tuushinde wakati?” Nikamwambia, kwa njia gani? Akasema: “Kwa majadiliano ya kifikira yenye manufaa.” Nikasema, ni kitu ambacho nakipenda sana katika maisha yangu, lakini ni lazima nijue jina lako na ujue jina langu. Akasema: “Sawa. Mimi ni Wahab.” Nikasema, na mimi ni Ali. Akasema: “Wewe ni madhehebu gani ewe Ali?” Nikasema mimi ni Shia. Akasema: “Na mimi ni Sunni wa madhehebu ya Wahabi, hakika ni miongoni mwa madhehebu.”

**Nikasema:** Ni lipi unalikusudia?

**Akasema:** “Madhehebu ya Wahabi.”

**Nikasema:** Unanifanyia mzaha?

**Akasema:** “Hapana, sikutanii.”

**Nikasema:** Basi niwie radhi, nimesema huenda umekosea.

**Akasema:** “Ni ya kweli ninayoyasikia! Una ujasiri kiasi hiki?”

**Nikasema:** Ndio ujasiri katika kupenda haki.

**Akasema:** “Kwanza nitakusimulia kuhusu jina la madhehebu yetu, lazima utakuwa hujasoma wala kusikia kuhusu sisi.”

**Nikasema:** Tafadhali.

---

## KUTAWASALI KWA MAWALII NA WATU WEMA

---

**Wahaab:** “Hakika mchipuo wa itikadi yetu ni mapito maarufu ya sheikh Ibnu Taymiyyah, mfano sisi hatuawili Aya za Qur’ani bali tunazichukulia kwa dhahiri yake, tunathibitisha aliyoyathibitisha Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Dhati Yake miongoni mwa mikono miwili, macho mawili, kuwa juu na kukaa, kama ilivyokuja katika Qur’ani tukufu katika kauli yake (s.w.t.): **“Mkono wa Mungu uko juu ya mikono yao,”**<sup>1</sup> na kauli Yake (s.w.t.): **“Naye yuko katika uwingu wa juu”**<sup>2</sup> na kauli yake (s.w.t.): **“Mwingi wa rehema amekaa juu ya Arshi.”**<sup>3</sup>

**Ali:** Hakika kuzichukulia Aya na Hadithi kwa maana ya matamshi yake bila ya kuzifanyia taawili ni jambo linalopingwa na akili sahihi kabla ya kila kitu na sira ya waarabu ambao walikuwa wakitumia matamshi katika maana yake ya majazi zaidi kuliko wanavyoyatumia katika uhakika. Imethibiti katika utafiti wa kitikadi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu sio mwili vinginevyo ingelazimu baadhi ya viungo kuhitajia baadhi yake na ingelazimu kuwa ni kiumbe kwa sababu viungo vyote vimeumbwa na yote hayo ni batili, hivyo makusudio ya *“yadullah”* ni maana ya majazi yaani uwezo wa Mwenyezi Mungu na *“Al-istiwau”* yaani, kutawala na kumiliki na *“ruuyatu”* kuona kwa moyo kuwa ni kutambua, vivyo hivyo katika majazi zilizo bakia.

---

<sup>1</sup> Suratul- Fatiha: 10

<sup>2</sup> Suratun Najim: 7

<sup>3</sup> Suratut Twaha: 5

**Wahaab:** Acha tujadiliane kuhusu tawhidi, kwani ndio msingi wa dini, hakika tawhidi kwetu ina vigawanyo viwili:

1. Tawhidi ya uungu: Yaani hakika Mola ndio Mwenyezi Mungu Mtukufu peke Yake hivyo tunampwekesha katika uungu Wake.
2. Tawhidi katika ibada: kwa maana kwamba ibada zote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Ali:** Haya maneno kila mwislam anayasema, na wala hakuna tofauti humo.

**Wahaab:** Ndio, lakini nyinyi mnamwabudu Mungu kwa wasila na hii ni aina ya shirki, hivyo haipatikani kwenu Tawhidi halisi.

**Ali:** Unakusudia nini katika wasila?

**Wahaab:** Kama vile wafu kati ya mawalii na watu wema, kwani nyinyi mnaifanya tawasuli kwao, na hii ni shirki katika ibada bali ni kufuru iliyo wazi.

**Ali:** Naomba unifafanulie maana ya shirki na kufuru kwenu na baada ya hapo nitakujibu kuhusu maudhui ya wasila.

**Wahaab:** Shirki kwetu iko aina mbili: Kubwa na ndogo. Kubwa ni shirki katika ibada mfano Shifaa, tawasuli kwa mawili na ndogo mfano kuapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu na ria. Na kufuru kwetu vile vile iko aina mbili: Kufuru halisi kwa Mwanadamu kufuru yote aliyokuja nayo Nabii (s.a.w.w.) na kufuru *muqayyad* nayo ni kukufuru baadhi ya aliyokuja nayo Nabii (s.a.w.w.).

**Ali:** Na waislamu kwa mtazamo wenu ni makafiri au washirikina?

**Wahaab:** Hakika wao bado wangali washirkina, kwa sababu wao hawamwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu isipokuwa kwa wastani, wasila na wanaapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu.

**Ali:** Hakuna kufuru *mutlaqa* na kufuru *muqayyadi* kama unavyodai kufuru ni mukabala wa imani na kufuru ni kutokuwa na imani ambayo mwenye kuwa nayo anakuwa muumini; na imani katika istilahi ni kusadikisha na kuamini yote aliyokujanayo Nabii angalau kwa ujumla na kwa hilo kufuru ni kukanusha aliyokujanayo Nabii (s.a.w.w.) na wala hapatikani kati ya waislamu leo anayemkanusha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).

Ama shirki yenyewe ina wigo mfinyu kuliko kufuru, nayo iko aina mbili:

1. Shirki katika dhati ya Mwenyezi Mungu - kuitakidi kuwepo waungu wawili au zaidi.
2. Shirki katika sifa za Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu kuitakidi kwamba kuna mwenye sifa kama za Mwenyezi Mungu.
3. Shiriki katika ibada ya Mwenyezi Mungu kwa kumwabudu pamoja na Mwenyezi Mungu mwingine au kumwabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu.
4. Shirki katika kutaka msaada - mwanadamu kumtegemea asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa namna ya pekee na kuitakidi kuwa anaathiri bila ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Aina zote hizi ni batili nazo ni katika shirki iliyoharamishwa, ama kutaka msaada kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa wastani (kama vile wafu, kati ya mawili na watu wema au mawasii) hiyo

sio shirki na iliyo mfano wake. Katika kisa cha Yusuf (a.s.) katika kauli yake (s.w.t.): **“Akamwambia yule ambaye alidhani atanusurika kati yao, nikumbuke kwa bwana wako.”**<sup>4</sup> Na hii ni alipotaka msaada kwa rafiki yake ambaye alikuwa pamoja naye katika jela kama alivyoeleza Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya hilo. Je, Nabii Yusufu atakuwa mshirikina kwa sababu alitaka msaada kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu? Ewe ndugu yangu, hakika Mwenyezi Mungu ameumba ulimwengu kwa wasta na sababu, na akajaalia kila kitu kulingana na kanuni hizi za jumla hata nusra za Manabii zilikuwa kulingana na kanuni hizi na wala sio kila mwenye kutaka msaada kwa sababu kati ya sababu hizi anahusishwa na shirki. Ama kutawasali kwetu hiyo ni kwa sababu wao wana daraja kubwa na tukufu kwa Mwenyezi Mungu na vile vile wana shifaa.

**Wahaab:** Acha tusimame kwenye shifaa kwa kuwa umeitaja vipi unaweza kuelezea maudhui ya shifaa pamoja na kwamba ni itikadi batili vipi Mwenyezi Mungu atamwandika mwanadamu kuwa ni katika watu wa motoni kisha muombezi anamtoa humo hii ni kinyume na elimu ya Mwenyezi Mungu.

**Ali:** Kwa nini mnaamini baadhi ya Aya na mnakufuru baadhi yake? Je, hujasikia kauli yake (s.w.t.): **“Siku hiyo uombezi hautafaa ila kwa yule anayemruhusu Mwenyezi Mungu tu na kuiridhia kauli yake”**<sup>5</sup> na kauli yake **“Nani awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake.”**<sup>6</sup> **“...na hawamuombei yeyote ila yule anayemridhia na kwa kumuogopa yeye wananyenyekea.”**<sup>7</sup> Na hadithi ambayo ni *mutawatir* kwa Waislamu wote hata Nabii anauombezi, aliomba kwawo na akakubaliwa “na maombi yangu yamejaaliwa kuwa ni uombezi wangu kwa umma wangu siku ya

<sup>4</sup> Suratut – Twaha: 109

<sup>5</sup> Suratut – Twaha: 109

<sup>6</sup> Suratut-Baqara: 255

<sup>7</sup> Suratul- Anbiyai: 28

Kiyama.”<sup>8</sup> Hivyo shifaa ni ruhusa itokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, atampa atakayemridhia kusema kwa atakayeruhusiwa, baada ya ruhusa hii ya Mwenyezi Mungu ya Shifaa imekuwa ni mahsusi kwa Nabii au Imamu na kwa ajili ya hilo tunamwomba. Muombezi hana athari yeyote kama si ruhusa ya Mwenyezi Mungu na mwombezi haombi kutengua kanuni ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu na wala uombezi wake haukhalifu elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu bali mwombezi anaomba:-

1. Kwa kushikamana na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu zinazopelekea kusamehewa.
2. Anaeleza sifa za mja zinazopelekea kusamehewa.
3. Au anaelezea sifa zake kwa ukaribu wake na Mwenyezi Mungu na utukufu wake kwake.

Hivi ndivyo inavyotimia shifaa. Hivyo sisi tunamwomba Nabii uombezi baada ya kukiri kuwa ni cheo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kisha Muhammad bin Abdul-wahab ametaja katika *Al-Hidayatus-Saniyah* katika risalatul-thaniyah: “Tunathibitisha shifaa ya Nabii wetu Muhammad siku ya Kiyama na kwa manabii wengine, malaika na watoto kulingana na ilivyopokelewa.”

**Wahaab:** Lakini ni vipi Nabii anageuza hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa wenye madhambi?

**Ali:** Shifaa ni mfano wa toba, hakika toba inabadilisha hali ya mwenye dhambi ili apate msamaha wa Mwenyezi Mungu, vivyo hivyo shifaa na maghufira.

**Wahaab:** Lakini msamaha na maghufira ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu na wala sio kwa mwingine.

<sup>8</sup> *Al-Bukhari* Juz. 11, Uk: 97 na *Muslim* Juz. 1, Uk: 190

**Ali:** Shifaa pia inatoka kwa Mwenyezi Mungu hujasikia Aya?

**Wahaab:** Ndio nimesikia, lakini wewe hujajibu maudhui ya kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

**Ali:** Imeshatokea kuapa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu katika sehemu nyingi katika Qur’ani tukufu nakutajia baadhi yake :

Kwanza - kiapo kilichotokea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu mfano (*Wal-asir*), (*Wal-Aadiyat*), (*Wanaaziat*), (*Wal-mursalat*), bali kubwa zaidi ni kauli yake (s.w.t.): (*Lau’mrika*) yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu anaapa kwa maisha ya Nabii (s.a.w.w.).

Pili – kiapo kilichotokea kwa Nabii (s.a.w.w.) kitendo na *taqiriri* (kukiri).<sup>9</sup> Imepokewa kutoka kwa Al-Bukhari kwamba alikuja mwanaume kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akasema, ni sadaka gani ni kubwa zaidi? Akasema naapa kwa baba yako, wewe unataka kutuambia kuwa unataka kutoa sadaka na wewe ni bakhili unaogopa ufakiri na una matumaini ya kubaki (milele). Na kwamba Nabii (saww) aliposikia kauli ya Ami yake Abu Twalib naye anasema: Mmesema uongo Naapa kwa nyumba ya Mwenyezi Mungu tumwache Muhammad, hali hatujapigana kwa ajili yake na kumtetea. Hakusema kitu chochote, na hii ni taqiriri yake (saww) kuruhusu kuapa kwa nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Tatu - kutoka kwa maswahaba, mfano kauli ya Amirul-Muumini-na Ali (a.s.) katika moja ya barua zake kwa Muawiya: “Naapa kwa maisha yangu kama utasema kwa akili yako bila ya matamano yako utanikuta mimi niko mbali mno miongoni mwa watu kutokana na damu ya Uthman.” Na imepokewa katika Muwatwa kauli ya Abu Bakr: “Naapa kwa baba yako usiku wako leo sio usiku,” na zote

<sup>9</sup> Maana ya taqiriri ya Nabii ni kwamba Nabii anashuhudia au anasikia kitu na wala hakipingi au kukikataza ambapo inamaanisha kuruhusiwa na uhalali.



hizi ni hoja, kisha ni juu yako kutambua kwamba kiapo hakimaani-shi ibada kwa ulichokiapia, bali ni kwa sababu ni kitukufu na kina heshimika, hakika sisi tunaapa kwayo kama alivyoapa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa viumbe Vyake kama vile kauli yake (s.w.t.): “*Wattiyini wazaytuni*” na kauli yake, “*watwariq.*” Kama Mwenyezi Mungu anaapa kwa tini na zaituni pamoja na kwamba ni kati ya vyakula vya kawaida je, sio haki kwetu baada ya hayo kuapa kwa kiumbe bora zaidi naye ni Nabii? Kwa kujua kwamba Maulamaa wa fiqih wamesema kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu hakuwajibishi - yaani - sio wajibu kujilazimisha nacho kisheria bali inajuzu kukhalifu.

**Wahaab:** Haya ni maneno mazuri lakini kimebaki kitu kimoja hatujakizungumza, maudhui ya mawalii.

**Ali:** Kipi hicho?

---

## KUAPA KWAO, KUZURU MAKABURI YAO, NA KUWEKA NADHIRI KWAO

---

**Wahaabi:** Je, huitakidi kuwa kutaka msaada kwa mawalii duniani pamoja na kuwa wao ni wafu ni jambo linalopingwa na akili na wala hailikubali? Tukiongezea kuwa hiyo ni dua kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu nayo ni haramu, kwa kauli Yake (s.w.t.): “Na wale mnaowaomba kinyume cha Mwenyezi Mungu hawawezi kuwanusuru wala hawawezi kunusuru nafsi zao. Hakika wale ambao mnawaomba kinyume cha Mwenyezi Mungu ni waja kama nyinyi.”<sup>10</sup> Na ni wazi Qur’ani imekemea jambo hili. Kwa nini mnawaomba watu wasiokuwepo?

**Ali:** Kwanza - mauti sio kumalizika kabisa kama unavyoona bali ni kuhama kutoka katika ulimwengu huu wakimaada kwenda katika ulimwengu mwingine nayo ni kutengana roho na mwili na wala sio kufa kwa roho: **“Na wala usiwaheسابu wale waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu bali wako hai.”**<sup>11</sup>

Pili – Nabii amehimiza itikadi hii kwa kauli na vitendo aliposema: “Tembeleeni makaburi hakika yanawakumbusha akhera.” Ameitoa An-Nasai katika *Sunan* yake, na Ibnu Maajah katika *Sunan* yake na Al-Ghazaali katika *Ihiyaul-Ulumi*. Na kwa kitendo chake (s.a.w.w.) alipotembelea makaburi ya mashahidi wa Uhudi na amezuru kaburi la mama yake, na akalia hapo kama ilivyo katika siira ya Ibnu Hishaam. Kama mauti ni kumalizika kabisa kwa nini Nabii aamuru kuzuru makaburi na kwa nini yeye mwenyewe anayazuru.

---

<sup>10</sup> Suratul-Aaraf:194

<sup>11</sup> Suratul –Al-Imran:169

Tatu – Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyeturuhusu hilo kwa kauli yake (s.w.t.): **“Enyi mlioamini, muogopeni Mwenyezi Mungu na takeni kwake wasila.”**<sup>12</sup> Na wasila hapa uko aina mbili:-

1. Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kwa amali njema. Na hapa hakuna mushikeli.
2. Tawasuli kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa watu.

Ya pili imegawanyika katika aina mbili:

1. Kabla ya mauti kama ilivyo katika kauli yake (s.w.t.): “Na lau walipodhulumu nafsi zao wangekujia na kumuomba Mwenyezi Mungu maghfira na Mtume akawaombea maghfira basi wangemkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe Mwenye huruma.”<sup>13</sup> Hii pia iko wazi.
2. Baada ya mauti: nayo inajuzu kwa yale uliyoyafahamu kwamba mauti sio kwisha na kwamba waislamu wote wanatekeleza itikadi hii na kama walivyosema: Dalili kubwa zaidi ni uwezekano wa kitu kutokea, na tumeshajua kwa uzoefu na hali halisi kwamba walii aliyekufa ana athari na ananufaisha na anaondoa madhara kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kama ni hivyo basi akili inatulingania kufanya tawasuli kwake.

Imepokewa kwamba Al-Mansuri alipohiji na kuzuru kaburi la Nabii (s.a.w.w.) alimuuliza Imam Malik akasema: “Ewe Abu Abdillah, nielekee Kibla na niombe au ni mwelekee Mtume wa Mwenyezi Mungu? Malik akasema: “Kwa nini ugeuze uso wako kwake naye

<sup>12</sup> Suratul- Maida :35

<sup>13</sup> Suratun-Nisai:64

ndiye wasila wako na wasila wa baba yako Adam kwa Mwenyezi Mungu, bali mwelekee ..... bali hata walahidi, wao pia wanazuru makaburi ya wakuu wao ili kuongeza nguvu zao za kiroho kulingana na madai yao.

Umeshajua awali kwamba itikadi yetu katika kuathiri mawalii inakuja baada ya idhini na ruhusa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama wanavyoathiri malaika. Sasa kuna kizuizi gani? Kila tatizo linaloweza kupatikana hapa linaweza kupatikana katika vitendo vya malaika vile vile. Ama aya uliyoitaja, “na wale ambao mnawaomba kinyume cha Mwenyezi Mungu hawawezi kuwanusuru” imeshuka kwa kushutumu kitendo cha washirikina ambao wanaitikidi kwamba masanamu yao ya mawe au wakuu wao wa kipagani wanaathiri athari inayojitegemea.

**Wahaab:** Ndio, naweza kuafikiana na wewe katika hilo, lakini unaitakidi kwamba walii aliyekufa anahitaji nadhiri? Je, huitakidi kwamba kuchinja na sadaka kwa mawalii inafanana na sadaka ambazo walikuwa wanazitoa washirikina kwa masanamu yao? Je, hiyo si shirki iliyo wazi kutoka kwenu pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: “Swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje kwa ajili yake”<sup>14</sup>. Hivyo kuchinja ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke yake.

**Ali:** Kwa hakika nadhiri ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake na wala hana mshirika, na sisi tunapochinja au kuweka nadhiri kwa mawalii (a.s.) kwa hakika ni nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lakini tunatoa zawadi thawabu zake kwao na wala sio zaidi. Ama waliyotolea dalili kwayo baadhi “swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje” kwamba aya inazungumzia kuchinja kuwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni makosa, kwani imepokewa katika lugha ya kiarabu kuhusu neno “*nahri*” maana yake ni kuelekea,

<sup>14</sup> Suratul –Kauthara: 2

waarabu wanasema (*manaaziluna tatanaahar*) yaani *tataqaabala* (yanaelekeana) na neno hili limekuja katika Aya kwa maana ya kunyanyua mikono hadi kwenye shingo kama ilivyopokewa kutoka kwa Maimam (a.s.).

Ama kuchagua baadhi ya sehemu kwa nadhiri ni kwa ajili ya kutaka utukufu wa sehemu ili thawabu za ibada ziwe nyingi zaidi kama ambavyo huchaguliwa baadhi ya sehemu takatifu kwa ajili hiyo. Haya, ingawa maana ya “*nahri*” iliyokusudiwa katika Aya ni kuchinja mnyama, na hili pia halina ubaya, kwani umeshajua kwamba sisi tunachinja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini thawabu za chinjo hili tunazotoa kwa ajili ya walii na tunafanya kwa jina lake kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Wahaab:** Lakini kabla hujaenda mbali narejea katika asili ya ziara ya makaburi, hakika ni mbaya kiakili kwa sababu inafanana na ibada ya washirikina kwa masanamu yao, kwa ajili hiyo Nabii (s.a.w.w.) amekataza kuyazuru na akakataza kufunga safari kuyaenda.

**Ali:** Nimekuambia mwanzo maiti sio kwamba hayupo bali ni kiumbe hai kwa vazi la akhera kisha Nabii (saww) amezuru kaburi la mama yake na kaburi la Ami yake Hamza na Fatma Zahara alizuru kaburi la Nabii kila siku, na Amirul-Munininina Ali (a.s.) alizuru kaburi la Nabii na kaburi la Fatma (a.s.).

As-Samhudiyy ametaja katika *Wafaul-Wafaai* kwamba Umar aliporejea kutoka katika Fatih Shaam, cha kwanza alichianza ni kwenda msikitini na kumsalimia Mtume, na kuwasili kwa Bilal kutoka Shaam kwa ajili ya kuzuru kaburi la Nabii (s.a.w.w.) bali hili ni ambalo waislam wameendelea kulifanya. Bali akili inalingania kuwatukuza waliotukuzwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na ziara ni aina ya kuwatukuza. Ama kauli yako kwamba ni aina ya ibada kama

vile ibada ya washirikina nakuambia kwamba kama kuzunguka ndio ambako kumefanya ziara kuwa shiriki basi waislamu wote ni washirika kwa sababu wao wanazunguka nyumba ya Mwenyezi Mungu, kama utasema tofauti ni makusudio na nia, basi waislamu wanamkusudia Mwenyezi Mungu hali ya kuwa wanazunguka nyumba tukufu “Al-Kaaba” Tunasema vile vile ziara yetu katika makaburi humo tunamkusudia Mwenyezi Mungu Mtukufu na hiyo ni tofauti na washirikina. Amepokea Al-Baihaqiy na Al-Ghazaliy kwamba Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Mwenye kunizuru anawajibika kupata shifaa yangu” na akasema “Mwenye kuhiji na wala asinizuru basi atakuwa amenipuuza” na amesema “Zuruni makaburi kwani yanawakumbusheni mauti.”

---

## KUJENGA MAKABURI NA KUYAPAM- BA

---

**Wahaab:** Ewe Ali niambie kwa nini mnajengea makaburi pamoja na kwamba kitendo hiki kimekhalifu sheria sahihi kwa kauli yake (s.a.w.w.): “Sitoacha kaburi lililojengewa isipokuwa nitalisawazisha.”

**Ali:** Kwanza: Sanadi ya hadithi ni dhaifu, bali mpokezi wake (Abu Hayaji) ambaye Ahmad bin Hanbali amesema juu yake kuwa: Amekosea katika hadithi mia tano na katika sanadi yake yupo Sufiyani Ath-Thauriy muongo na yupo Abu Waili naye ni mwenye kumchukia Ali (a.s.).

Pili: Ama matini ya Hadithi hakika tamko (*tasiwiyatu*) linamaanisha wastani kati ya kunyanyuka sana na kuvunja kwa kufuta kabisa na dalili ni kwamba sheria ya kislamu imeleta sunna ya kunyanyua makaburi shibiri moja au vidole vinne kutoka usawa wa ardhi, hivyo sheria inakubali kujengea kwa kunyanyuka kutoka ardhini kwa kiasi hiki na hadithi uliyoitolea ushahidi haifungamani na kutoruhusu kujengea abadani.

Tatu: Tunasema sio Shia tu peke yao ambao hujengea makaburi, hili kaburi la Nabii Ibrahim (a.s.) nchini Jordan lina kuba, na dharihi (kaburi) la Musa (a.s.) nchini Jordan baina ya Qudus na Aman lina jengo kubwa. Kaburi la Abu Hanifa huko Baghdadi, kaburi la Abu Huraira huko Misri, kaburi la Abdul-Qadir huko Baghdad, tukiachilia mbali makaburi ya Wafalme na wakuu, na hakupinga majengo haya yeyote kati ya Waislamu hivyo inajuzu kwa asili.

Nne: kujengea makaburi ya Manabii, Mawalii na Wakuu ni dalili ya umma kuwajali hao watukufu na kuelekeza watu kwao na

kuwaunganisha wao kwa kupitia dharihi hizo, kuyajali makaburi kunawakilisha hali ya maendeleo ya jamii na kudumisha kumbukumbu ya watu wema na kuhifadhi historia ya umma.

**Wahaab:** Lakini hamtosheki kujengea tu bali mnatumia mali nyingi kuyapamba makaburi haya, kuna mapambo mbalimbali na hii ni haramu kabisa kwa sababu ni isirafu iliyo wazi pamoja na kutokuwepo haja ya walii kwayo na wala hanufaiki kwayo.

**Ali:** Kama upinzani wako kwa mapambo ya dhahabu na taa na vitu vingine ambavyo vimepambiwa makaburi ya Manabii na Maimamu (a.s.), utasemaje kuhusu pambo la Al-Ka'aba ambalo lina thamani ya mamilioni? Kama upinzani wako kwa kupamba kaburi la maiti asiyefaidika nayo hali kadhalika pambo la Al-Ka'aba ambalo hubadilishwa kila mwaka na vile vile zawadi za thamani zilizokuwa zinatolewa wakati wa ujahilia katika nyumba ya Mwenyezi Mungu na hadi leo, kwani Mtume (s.a.w.w.) alipata wakia sabini za dhahabu akaambiwa ni vema ungezitumia katika vita vyako lakini hakufanya hivyo na akaziacha katika hali yake vile vile khalifa wa kwanza, hili pambo ni namna ya kuonyesha utukufu nayo ni alama kati ya alama, na mushkeli wowote unaopatikana katika makaburi ya Mawalii basi vivyo hivyo katika kupamba nyumba ya Mwenyezi Mungu tukufu pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu hana haja nayo, kisha sisi hatudai kuwa maiti hafaidiki nayo kama unavyodai wewe bali ni mkusanyiko wa hidaya na hizo hufanya mambo kuwa mepesi kwa wanaozuru mfano kuwepo umeme n.k.



---

## MAJINA YA KUUNGWA

---

**Wahaab:** Ukungu umeanza kuniondokea kidogo kidogo, lakini ewe Ali, nina swali kuhusu majina ya kuyaunganisha kwenu mfano (Abdul–Husein, Abdu Ali, Abduz–Zahara), haya yanathibitisha ibada kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Ali:** Ama kuhusu majina ya kuunganisha hakika tamko Abdu halimaanishi kuabudu bali lina maana nyingine isiyokuwa hiyo, mfano wa kauli yako (*Zayd A'bdu fulani*) na (*fulanah amatu fulanah*) kauli hii inatumika kwa waraabu haimaanishi kwamba Zayd anamwabudu bwana wake fulani bali inamaanisha kuwa yeye yuko chini ya milki yake na wala si vinginevyo. Tunapomwita (Abdul–Husein) hatokusudii kwamba yeye anamwabudu Husein bali ni katika upande wa kuwaheshimu watukufu kama ambavyo Zayd alikuwa ni Abdun – Nabii kisha akamwacha huru.

---

## KUSUJUDU JUU YA TURBA

---

**Wahaab:** Kama hamkuwa mnamwabudu Husein kwa nini mnaabudu turba yake na mnasujudu juu yake?

**Ali:** Kusujudu juu ya turba haina maana ya kuiabudu kama ulivyodhani. Ili iwe wazi kwako nakuambia:

- a. Haiwezekani mwanadamu kusujudu juu ya anachoki-abudu, hilo ni jambo lisiloingia akilini hivyo sisi tunasujudu juu ya turba kwa kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- b. Sijda hii ni mubaha katika sheria ya kiislamu, pande zote za kiislamu zimepokea hadithi hii. “Nimejaaliwa ardhi kuwa mahali pa kusujudia na ni tohara,”<sup>15</sup> hivyo udongo tohara inajuzu kusujudu juu yake kwa sababu ni katika ardhi. Na sisi tunasujudu juu ya udongo tohara, na kwa tahadhari zaidi na wepesi wa kuhamishika imetengenezwa turba kwa muundo huu.
- c. Ama kuhusu turba ya Husein, imepokewa katika Sunna kwamba Ardhi baadhi yake ni bora kuliko nyingine kama vile kauli ya Nabii (s.a.w.w.): “Swala katika masjid mbili ni sawa na (swala elfu katika isiyo kuwa hiyo). Na hadithi hii ni *mutafaquni alaihi*, na hii imekuja kwa shakhsia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kutukuzwa na Mwenyezi Mungu, hivyo kila mtu mtukufu inatukuka sehemu ambayo amezikwa humo, hivyo Husein ni bwana wa vijana wa watu wa peponi na ni bwana wa mashahidi aliyejitoa muhanga wa damu yake, familia yake na wafuasi wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hivyo ni kati ya watukufu

---

<sup>15</sup> *Sahih Bukhari*, kitabu tayamamu Jz: 1, na *Sunanul-Kubra* Jz: 2

walioitukuza ardhi. – Na kusujudu juu ya turba ya Husein ni kwa sababu – Karbala – ni kati ya ardhi takatifu kama ambavyo zimepokewa riwaya nyingi kwetu.

---

## KUBUSU DHARIHI

---

**W**aahab: Lakini Ewe Ali, jambo ambalo huwezi kulikataa ni kubusu makaburi ya mawalii wema na kuswali humo, hii imepingwa kwa upande wa kisheria, nayo ni haramu kwa upande mmoja na ni shirki kwa upande mwingine.

**Ali:** Kubusu ni hali ya kibinadamu na ina maana nyingi, kati ya hizo ni:-

- Baba kumbusu mtoto wake.
- Rafiki kumbusu rafiki yake na vile vile kubusu Qur’ani tukufu, Jiwe Jeusi, kaburi na sehemu takatifu.

Kwanza, ni kuonyesha mapenzi kwa mtoto na rafiki.

Pili, ni kuonyesha utukufu, kama kubusu ni shirki basi inakatazwa ambapo itabidi baba awe mshirikina kwa kumbusu mtoto wake, na kama aina ya pili ndio shirki basi tunasema: Waislamu wote ni washirikina kwa sababu wao wanabusu Jiwe Jeusi na Jalada la Qur’ani, bali Ibn Bazi amesema katika *Atahaqiyqu wal-Idhaahi*, Uk: 41: “Kisha liendee jiwe jeusi na lielekee kisha ulishike kwa mkono wako wa kulia na ulibusu kama itawezekana.” Huyo ni mufti wa wahabi ameruhusu kubusu Jiwe Jeusi na hakuna shaka kwamba makusudio ni kulitukuza na kutabaruku, kadhalika kubusu makaburi ni kuwatukuza na wala sio kuwaabudu. Sisi hatuwali kwa ajili ya makaburi bali tunaswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na unaweza kufika katika makaburi ya mawalii ili uone tunaswali kwa ajili ya nani?

**Wahaab:** Hivi sasa sijui nisemeje kwani umeshanifafanulia mambo mengi muhimu kuhusu yale ambayo watu wengi wanasema ni bidaa.

**Ali:** Acha nikukate kauli ili nikufafanulie maana ya bidaa. Bidaa kwa baadhi ya watu ni kuzua mambo ambayo hayakuwepo wakati wa Nabii (s.a.w.w.) na maswahaba mfano – ukumbusho ambao unaletwa kabla ya adhana, kusoma kaswida katika maulidi ya Nabii na Maimam (a.s.) tasibihi, kuchomekea, kuvaa tai, na mfano wa haya kama vile Shia kuomboleza, kujengea makaburi na mengineyo ambayo tumeshayazungumza kwa pamoja, yote haya baadhi ya watu wanayazingatia kuwa ni bidaa.

Lakini kwa hakika bidaa ni kuingiza yasiyokuwa dini katika dini, kama vile kuhalalisha kilichoharamishwa au kuharamisha kilichohalalishwa au kuyafanya wajibu yasiyokuwa ya wajibu au kuyafanya Sunna yasiyokuwa ya Sunna. Mfano kubusu mkono wa mwanachuoni kwa lengo la kumheshimu na kumtukuza kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu inajuzu hata kama haikuwepo wakati wa Nabii (s.a.w.w.) na maswahaba na wala hakujapokewa juu yake Nnasi, baada ya kuwa kwake ni aina ya heshima kwa ada na inafahamika kutokana na sheria kupendeza kwake katika kumheshimu muumini kuwa inajuzu au inapendeza, vile vile maulidi na nyuradi hakika ni katika upande wa kumtukuza aliyetukuzwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumsifu aliyesifiwa na Mwenyezi Mungu kama ambavyo baadhi ya maulana wanahalalisha kuwasifu wafalme basi ni vivyo hivyo katika maulidi na maombolezo tukiachilia mbali kwamba baadhi ya mambo haya yalikuwepo wakati wa Nabii (s.a.w.w.), mfano kusifu kwa haki au kulia na kuomboleza kama ilivyotokea wakati wa kufa shahidi Hamza, kuzaliwa kwa Husein (a.s.), kufariki kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) n.k.

Ama masahaba ni watu wa kawaida; tena wala sio maasum hadi tutoe hoja kwa vitendo vyao kama tunavyotoa hoja kwa vitendo vya Nabii, kati yao kuna wema na waovu na wala sio kila asichokifanya Swahaba kinakuwa haramu wala sio kila alichokifanya Swahaba ni wajibu au halali, baadhi ya mambo hayakuwepo wakati wa Nabii wala katika wakati wa maswahaba lakini yanajuzu na ni mubaha, mfano kuvaa suruali, tarabushi na vingi kati ya vyakula vya kisa-sa vilivyo halali ambavyo havikuwepo wakati wao hivyo haisemi kuwa ni bidaa. Natija ni kwamba yaliyothibiti kupendeza kwa ujumla (mfano kumheshimu muumini) ambapo inalazimu kwa aina yake na wala sio kwa umahsusi haiwi bidaa.

---

## MASAHABA WANGU NI KAMA NYOTA

---

**Wahaab:** Lakini kuna Hadithi ya Mtume (s.a.w.w.) inasema, “masahaba wangu ni kama nyota yeyote mtakayemfuata mtaongoka.”

**Ali:** Kwanza sanadi ya Hadithi hii ni dhaifu mno kwa sababu mpokezi wake ni Abdur-rahim bin Zayd na Hamza bin Abiy Hamza al-Jaziry na Harith bin Adhiyn. Ama Abdar-rahim ametuhumiwa na wachambuzi wa hadithi kwa udhaifu wake na umashuhuri wake kwa uongo na kutokuwa mwaminifu, na unaweza kurejea (*Tahadhiybut-Tahadhiyb*) Juzuu ya sita. Ama Hamza ametuhumiwa na ni maarufu kwa uongo na ubovu wa hadithi na kuongezea riwaya na unaweza kurejea kitabu kilichotajwa Juzuu ya tatu. Ama Harithi ha-julikani, na wala haijuzu kupokea riwaya kwa asiyejulikana na kuzitegemea, na unaweza kurejea *Lisanul-Mizani* cha Al-Asqalaaniy Juzuu ya pili. Na maulamaa wengi wa Ahlus-Sunna wanasema juu ya uongo wa hadithi hii, kati yao ni Ibnu Hazim al-Andalusiy, na unaweza kutazama maneno yake katika *Al-Baharul-Muhiyt*. Na Abu Bakri Al-Bazazi utakuta maneno yake katika kitabu *Jamiul-bayaanililiimi* cha Qurtubiy na Ahmad bin Hanbali katika kitabu chake *Al-Taqiriru watahbiru* cha Halabiy, kwa hiyo haiwezekani kutolea ushahidi kwa hadithi hii kwa yale uliyoyasikia kwa hiyo sio kila swahaba ni mwadilifu kwa sababu wao sio nyota.

---

## SHAHADA YA TATU

---

**Wahaab:** Nitarejea tena katika maswali ya maswahaba baadaye, lakini limebaki swali kuhusu shahada ya tatu ambayo mnaitaja katika adhana na iqama, lakini haikuwepo wakati wa Nabii (s.a.w.w.) hiyo ni bidaa na wala hakuna mushikeli.

**Ali:** Kwanza Ali (a.s.) yeye ni nafsi ya Nabii (s.a.w.w.) kwa dalili ya aya ya mubahala “**Nafsi zetu na nafsi zenu**” na makusudio ni Ali na Nabii na kizazi chao pamoja na hivyo hakuna kizuizi kutaja jina lake pamoja na yaliyopokewa kutoka kwa Nabii kauli yake kwa Ali “Hakika yeye anatokana na mimi, na mimi ninatokana na yeye” imepokewa na pande zote mbili.

**Pili** – Hakika Ali (a.s.) ni bwana wa waumini baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kama alivyosema (s.a.w.w.): “Wewe ni kiongozi wa kila muumini baada yangu.”<sup>16</sup> Hivyo kumtaja katika adhana na iqama kwa anuani ya kuwa kwake walii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuna kikwazo abadani.

**Tatu:** Tuna riwaya katika upande wetu zinazotuamrisha kutaja shahada ya tatu ya Ali kila inapotajwa shahada ya Nabii (s.a.w.w.), mfano kauli yake (s.a.w.w.): Atakaposema mmoja wenu Lailaha ilallah Muhammad Rasulu Ilaahi basi aseme Aliyaan Amirul-muminina. Na kutoka kwake (s.a.w.w.) amemwambia Ali: “Ewe Ali, nimemuomba Mola Wangu utajwe ninapotajwa basi akanikubalia, imekuja kutoka kwa Imam wetu As-Swadiq (a.s.) amesema: Tawhidi ni “Lailaha illa Ilahu Muhammada Rasullu Ilahi Aliyun Amirul-muuminina.” Kutokana na dalili hizi na nyinginezo tunataja shahada ya tatu ya uwalii wa Ali kama ilivyo Qur’ani katika kauli

<sup>16</sup> *Fadhails-Swahaba* cha Anasayi na *Sunnaul-Kubra*, Juz: 5 na *Maswabih Sunnah* J:1



Yake (s.w.t.): “Hakika kiongozi (wali) wenu ni Mwenyezi Mungu, Mtume wake na wale walioamini, ambao wanasimamisha swala na wanatoa sadaka hali ya kuwa ni wenye kurukuu.”<sup>17</sup>

Aya hizi zimeshuka wakati Amirul-Muuminina Ali alipotoa sadaka pete yake naye yuko katika Swala basi neno (kiongozi wenu) limekuja kufafanua kuwa Ali (a.s.) ni kiongozi wa watu.

---

<sup>17</sup> Suratul- Maida: 55

---

## KUKUSANYA BAINA YA SWALA MBILI

---

**Wahaab:** Vema swali langu la mwisho ni juu ya dalili ya kukusanya baina ya Swala mbili ambayo mnafanya.

**Ali:** Madhehebu matatu ya Maliki, Shafii na Hanbali yanaafiki-ana juu ya kujuzu kukusanya Swala mbili katika safari na wamehitafiana katika kujuzu hilo pasipokuwa na safari kama vile maradhi na hofu. Ama dalili ya Shia katika kujuzu kukusanya Swala katika safari na pasipo safari ni:

1. Kauli Yake (s.w.t.): **“Simamisha Swala linapopinduka jua hadi giza la usiku na Qur’ani ya Alfajiri, hakika Qur’ani ya alifajiri ni yenye kushuhudiwa.”**<sup>18</sup> Aya inataja nyakati tatu katika kusimamisha Swala: Jua linapopinduka, nayo ni Adhuhuri na Alasiri, na *duluki shamsi* yaani kupinduka kwake kutoka katika nusu ya mchana, *ilaa ghasaqi laili* nao ni wakati wa kumalizika kwa wakati wa Swala ya magharibi na Isha na ghasaq ni giza nene, *walfajiri* ni wakati wa Swala ya asubuhi.
2. Kauli Yake (s.w.t.): **“Simamisha Swala ncha mbili na giza la usiku hakika mema yanaondosha mabaya, huo ni ukumbusho kwa wenye kukumbuka.”**<sup>19</sup>

Aya hii vile vile inataja nyakati tatu kwa ajili ya Swala, nazo ni: *twarafay nahaar* - ncha ya kwanza ni mwanzo wa Swala ya asubuhi, na ncha ya pili ni linapopinduka jua hadi magharibi nao ni wakati

---

<sup>18</sup> Suratul Israa: 78

<sup>19</sup> Suratul Huud:114

wa swala ya Adhuhuri na Alaasiri, *wazulafan minalaili* - ni wakati wa kushirkiana baina ya Swala mbili Magharibi na Isha.

3. Na kuna Hadithi nyingi zilizopokelewa katika kubainisha hayo na kujuzu kwake. Kutoka kwa Ibnu Abbasi amesema: Aliswali Mtume (saww) Madina Adhuhuri na Alasiri pasipo hofu wala safari akaambiwa kwa nini umefanya hivyo? Akasema ametaka asimfanye uzito yeyote katika umma wake,<sup>20</sup> na kutoka kwake: Hakika Nabii (s.a.w.w.) aliswali Madina Adhuhuri na Alasiri 8 na 7 kwa magharibi na Isha,<sup>21</sup> na nyinginezo katika hadithi zilizopokelewa kwa njia za kisunni, ama katika rejea zetu mambo yako wazi, tuna riwaya nyingi za Ahlul-Bait kuhusu kujuzu kukusanya baina ya Swala mbili.

**Wahaab:** Nakushukuru ewe ndugu yangu, umenipa mwanga sana naomba unieleze baadhi ya rejea ambazo zinadhihirisha ukweli.

**Ali:** Sawa kabisa kuna ambao wamejibu na wamempinga Muhammad bin Abdul-Wahabi kati ya maulamaa wa Kisunni na Shia nakutajia wafuatao:-

1. Ndugu yake Suleimani bin Abdul-Wahabi katika kitabu chake *Faswilul-Khitab fiy radi alaa Muhammad bin Abdul-Wahaab*.
2. Abdilah bin Isa as-Swana'aniy katika *as-Saiful-hindiy fiy ibaanati twariqatis-shaykhinajidiy*, na kitabu chake kingine *As-Saiful-baatiru fiy unuqil-munkir alaal-akaabir*.
3. Yusufu An-Nabahaaniy katika *Shawaahidul-Haqi fiy tawasuli bisayidil-Khalqi*.

<sup>20</sup> *Sahihi Muslim*, Babu jamui baina swalatayni

<sup>21</sup> *Sahihul-Bukhariy* babu taakhir Dhuhur ilaa-Asir katika kitabu cha *ma waqitis-Swalaat*.

4. Ahmad bin Zayn Dahalaan Mufti wa Makka katika *Futu-haatil-Islaamiyah*.
5. Muhammad bin Suleiman Al-Kaurdiy As-Shaafiy.
6. Atwaul-Makkiy katika *Aswaarimul-Hindiy fiy unuqin Najidiy*, na wengineo wengi.

Na katika Shia tazama *Kitabul-Jaamiu Kashiful-Iritiyaab* cha Muhsinul-Aminiy na *Hadhihi hiyal-wahabiyah* cha Muhammad Jawwad al-Mughuniyyah, *Hadhihi hiya Shia* cha Baaqir Shariyf al-Qarashiy na vinginevyo.

---

## TAQIYYA

---

**Wahaab:** Vizuri ewe Ali ....Waislam wanaitakidi kuwa itikadi ya taqiyya ambayo mmejilazimisha nayo ni aina nyingine ya unafiki au uongo ambao mmejificha nyuma yake, na baadhi wanaitakidi kwamba Shia wametumia silaha hii walipobanwa na udikteta wa Bani Umayya na wengineo... lakini kwa kweli taqiyya inahesabiwa kuwa ni unafiki katika dini na imani.

**Ali:** Unasemaje? Hakika *taqiyya* ni mafuhumu ya Qur’ani na dini ambayo ameianzisha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Wahaab:** Nini? Wapi na lini? Na kwa nini hawajui hayo zaidi yenu?

**Ali:** Kabla sijakujibu maswali yako napenda kukufahamisha maana ya taqiyya. *Taqiyya* ni neno lililotokana na *wiqaaya* na makuudio yake ni kujilinda na madhara ya wengine kwa kuwaafiki kwa kauli au kwa kitendo. Na lengo lake ni kuhifadhi nafsi, heshima na mali katika nyakati ngumu ambazo muumini humo hawezi kudhihirisha msimamo wake wa haki wazi wazi, na hiyo ni silaha dhaifu mbele ya nguvu ya dhulma, yaani ni silaha ya mwenye kukabiliwa na mtu ambaye haheshimu damu yake, utu wake na mali yake. Kwa ajili hii inakubainikia wazi ewe Wahaab hakika taqiyya ni kama vile ngao, nalo ni jambo la kimaumbile anaweza kulifanya binadamu yeyote, lakini kwa anuani nyingine. Ama wapi tunapata dalili za Qur’ani zilizokuja kwa taqiyya kama ulivyouliza ni hizi:

Amesema Mwenyezi Mungu: **“Mwenye kumkufuru Mwenyezi Mungu baada ya kumwamini kwake isipokuwa mwenye kulazimishwa na moyo wake umetulizana kwa imani.”**<sup>22</sup> Kwa kon-

---

<sup>22</sup> Suratun Nahli: 106

gamano la wafasiri imeshuka kuhusu kadhia ya Ammar bin Yaasir alipopatwa na mateso makali kutoka kwa makuraishi na wakambana awasifu waungu na amshutumu Nabii (s.a.w.w.). Ammar akasema hayo dhahiri isipokuwa moyo wake ulitulizana kwa imani ili azuie mateso (na alipomjulisha Nabii hali halisi ilivyokuwa, akamwambia wakikulazimisha tena fanya hivyo hivyo), na Shaafiy na Maaliki wana kubali kujuzu kwa taqiyya.<sup>23</sup>

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa marafiki kinyume na waumini, na atakayefanya hivyo sio chochote kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa mkiogopa kwao madhara,”**<sup>24</sup> na kubagua huku (isipokuwa) maana yake inajuzu kwa muumini kumfanya kafiri kuwa rafiki katika hali na nyakati za dharura na ngumu katika upande wa taqiyya kama alivyosema hayo Twabariy, Zamakhshariy, Raaziy, Al-Aluusiyy na Al-Maraaqiy katika tafsiri zao kuhusu Aya hii.

**Wahaab:** Sikujua kabisa katika maisha yangu yote maana ya Aya hizi asilani, umenipa mwanga ewe Ali, lakini.....

**Ali:** Lakini nini, Sema?

**Wahaab:** Lakini huitakidi kuwa aya hizi na nyinginezo zinahusu taqiyya na makafiri tu, na nyinyi Shia mnafanya taqiyya pamoja na makafiri na wasiokuwa makafiri?

**Ali:** Nimeshakuambia ewe Wahaab kwamba, lengo la sheria ya taqiyya katika Qur’ani ni kulinda nafsi, mali na utu, popote mwislam atakapopatwa na hofu hii anaweza kufanya taqiyya, na wala sio mahsusi kwa makafiri, inaweza kuwa baadhi ya waislam ni madhalimu zaidi kuliko makafiri kama yalivyotokea hayo katika dola ya Bani Abbas.

<sup>23</sup> Tazama tafsiri zifuatazo- *Al-Kaashif* ya Zamakhshariy Jz: 2, uk: 430, Jamiul-Ahkaamil-Qur’ani Jz: 4, uk: 57, na *Tafsirul-Khaazin* uk: 277.

<sup>24</sup> Suratul-Imraan:28

**Wahaab:** Je ninaweza kuacha swala kwa anuani ya taqiyya au kuuwa mwislamu kwa taqiyya vile vile?

**Ali:** Hapana, asilani... kuna sehemu ambazo hakuna taqiyya humo kwa yeyote na vyovyote itakavyokuwa kama vile kuvunja dini, kuficha ukweli, kupotea kwa kizazi na kusaliti mambo ya waislam kwa maadui, maulamaa wetu wamesema hakuna taqiyya katika kumwaga damu. Kwa kifupi ni kwamba taqiyya haiwi katika mambo ambayo yanasababisha uharibifu.

**Wahaab:** umenifahamisha mambo ambayo yalikuwa hayafahamiki kwetu ewe Ali, ubarikiwe kwa ajili yangu ewe Ali.

**Ali:** Hakuna shukurani katika kufanya wajibu, je sasa imebakia kwako swali lolote?

**Wahab:** Ndio, bila shaka kila unapoingia katika mazungumzo na mimi yananijia baadhi ya mambo akilini mwangu napenda kuyasikia kutoka kwako.

**Ali:** Vema ni yapi hayo?

---

## UMAASUMU

---

**Wahaab:** Nyinyi Shia mnaitakidi ulazima wa umaasum wa Nabii na Imam wapi mmeutoa ulazima huu?

**Ali:** Katika akili na Qur’ani. Ama dalili ya kiakili ni kwamba Nabii (s.a.w.w.) au Imam analinda sheria tukufu na lengo la kutumwa kwake ni kuongoza watu na kuwafikisha katika ukamilifu, na wala haiwezekani kuihifadhi kama sio maasum vinginevyo ikiwa ni kinyume maana yake ni kwamba anaweza kukosea au kusahau katika mambo ya kisheria hii ina maana kutotimia lengo la kuongoza kwa ukamimlifu, na dini kutotosheleza maisha, na kwa hiyo lengo la Mwenyezi Mungu ambalo kwalo amentuma Nabii ni lenye kupotea na kutotimia. Na kama lengo hili halitotimia tutasemaje ni Mungu kashindwa? Ambapo hakuweza kumlinda Nabii? Na jawabu ni Hapana, bali yeye ni Muweza na ni Mjuzi. Kama hivyo ndivyo, basi ni wajibu kwake kumfanya Nabii au Imam kuwa ma’asum.

**Wahaab:** Je umaasum unapokonya hiyari ya Nabii au Imam?

**Ali:** Hapana abadani, bali iko chini ya hiyari yake kwa sababu kutenzwa nguvu kwa aina zake zote ni batili kwetu.

**Wahaab:** Nifafanulie hayo.

**Ali:** Uma’asum una maana ya kulingana nguvu zote kwa mwanadamu na akili kutawala nguvu zote hizi zinazowiana, ambapo kunapatikana mtazamo wa kina wa kiakili kwa Nabii (s.a.w.w.) katika matarajio yote ya Nabii, matakwa yake, mategemeo yake na hisia zake, na chini ya kivuli hiki cha upevu wa kiakili, vipawa vizuri vinakamilika miongoni mwa ukweli, kutimiza ahadi, subira, uaminifu na .... na huu ndio uma’asum, kisha unaongezwa katika haya wahyi ambao unaipa nguvu Nubuawah na Imamah.



**Wahaab:** Ni wapi Nabii anapata upevu huu wa kiakili na maendeleo ya kiroho?

**Ali:** Hakika ni mkusanyiko wa misimamo yake, kuikanya kwake nafsi yake katika matamano yake, kuepuka kwake shari, usafi wa nafsi yake, matakwa yake na kupenda kwake kheri daima, na ambayo yanatokana na Mwenyezi Mungu humea na kukua.

**Wahaab:** Je katika Qur’ani kuna dalili juu ya ismah?

**Ali:** Ndio, amesema Mwenyezi Mungu: **“Hatamki kwa matamano yake isipokuwa ni wahyi unaofunuliwa.”**<sup>25</sup> Mola wetu anatuambia kwamba Nabii (s.a.w.w.) hatamki katika maisha yake yote isipokuwa ni wahyi na hii inamaana ya uma’asum na haki. Na amesema (s.w.t.): **“Hakika anataka Mwenyezi Mungu kuwaondolea uchafu Ahlul-bait na kukutakaseni kabisa.”**<sup>26</sup> (kuwaondolea) yenye kuendelea kwa sababu ni kitendo kilichopo, (uchafu) wote wa kimaada na wa kimaanawiy (Ahlul-bait) Nabii na Ahlul-bait wake na (kuwasafisha) kutokana na uchafu wote wa kimaada na wa kimaanawiy ina maana ya umaasum, na nyinginezo kati ya Aya za Qur’ani.

**Wahaab:** Ndugu yangu nakuomba unieleze wazi katika swala hili.

**Ali:** Je, umenikuta niko kinyume na hivyo?

<sup>25</sup> Suratun Najim: 3-4

<sup>26</sup> Suratul - Ahzab: 33

---

## KUPOTOSHWA KWA QUR'AN

---

**Wahaab:** Hapana, sikukusudia hilo, lakini nataka ukweli, je Shia wana Qur'ani nyingine isiyokuwa Qur'ani iliyopo kwa Waislam?

**Ali:** Hapana ewe ndugu yangu, ni propaganda na tuhuma wanatusingizia baadhi ili kupotosha, na mimi nashangaa kwa ambao wanaamini hayo! Je hawaoni misikiti ya Mashia na nyumba zao, hakika wao wanasoma Qur'ani hii iliyopo na wala haipatikani isiyokuwa hiyo.

**Wahaab:** Wanasema nyinyi mna Qur'ani inayoitwa Msahafu wa Ali au Msahafu wa Fatma?

**Ali:** Wewe unajua kwamba neno msahafu lina maana ya ambayo yamekusanywa katika jalada mbili nalo ni neno linalotumiwa kwa isiyokuwa Qur'ani vile vile, lakini kwa wingi wa matumizi yake katika Qur'ani limekuwa ni mahsusi kwayo. Ama msahafu wa Ali au wa Fatma una maana ya kitabu cha Ali au Fatma hiyo sio Qur'ani ambayo ni mukabala wa Qur'ani hii. Bali msahafu wa Fatma ni kitabu ambacho kimekusanya mambo ya vita na fitina, amerithi baadhi ya hayo kutoka kwa baba yake Mtume (s.a.w.w.) nayo ni mas'ala ya kawaida, ama msahafu wa Ali ni Qur'ani hii hii lakini ameandika pembezoni mwake tafsiri na taawili ya kila aya ni hivyo tu, pamoja na kwamba sisi leo hatuna vitabu hivyo viwili bali tunaitakidi kuwa viko kwa Imam Al-Mahdy (a.s.).

**Wahaab:** Vema, je mnaitakidi kuwa Qur'ani hii imepotoshwa au laa?

**Ali:** Hapana haikupotoshwa, kwa kauli yake (s.w.t.): **“Hakika sisi tumeteremsha Qur’ani na sisi ni wenye kuilinda.”**<sup>27</sup>

**Wahaab:** Wanasema kuwa nyinyi mna riwaya kutoka kwa Maimam zinazoeleza wazi kupotoshwa kwa Qur’ani.

**Ali:** Ndio mimi sikatai hilo, lakini riwaya zinazungumza juu ya kupotoshwa maana ya Qur’ani na wala sio kupotosha matamko ya Qur’ani mfano: sisi tunaitakidi kwamba maana ya (**Ulul-amr**)<sup>28</sup> in- amkusaidia Ali na watoto wake wakati ambapo baadhi wamesema inakusudia *Ahlul-hili wal-uqud* hii ni aina kati ya aina za kupotosha maana, sisi tunakiri usalama wa Qur’ani kutokana na ziada na upun- gufu, lakini tunaitakidi kupotoshwa maana zake, lakini nimekuam- bia ewe Wahaab hakika baadhi ya waislam walikuwa wanaitakidi kupotoshwa kwa Qur’ani wasiokuwa Shia.

**Wahaab:** mfano nani?

**Ali:** Kati yao ni Umar bin Khattabb na Aisha.

**Wahaab:** Ni nini dalili yako juu ya hilo?

**Ali:** Umar bin Khattab amesema: “Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alimtuma Muhammad (s.a.w.w.) kwa haki, na akateremsha kwake Kitabu, na ilikuwa kati ya yaliyoteremshwa kwake ni Aya ya *rajim*.”<sup>29</sup>

Na Aisha amesema: “Ilishateremka Aya ya rajim na kunyonye- sha mtu mzima mara kumi na ilikuwa katika karatasi chini ya kitan- da, alipofariki Mtume (s.a.w.) tukashughulika na mauti yake, mbuzi akaingia na akaila.”<sup>30</sup> Sasa iko wapi aya ya rajim? Hakika haipati- kani katika Qur’ani, hii ina maanisha kumpinga kwake - Mwenyezi

<sup>27</sup> Suratul-Hijir: 9

<sup>28</sup> Suratun Nisaa: 59

<sup>29</sup> *Tarikh-Twalib* Juz. 2, Uk: 235 Hadith ya Saqifah na *Tarikh Al-Yaaqubiy* Juz. 2, Uk :160

<sup>30</sup> *Hayatul-Hayawaan cha Damiry* Juz. 1 Uk: 275

Mungu atulinde. Vipi hakuiona aya hii isipokuwa Umar na Aisha, wako wapi waandishi wa wahyi? Je, huitakidi kuwa riwaya hizi ni hatari sana ewe Wahaab?

**Wahaab:** (Akanyamaza na kushangaa aliyoyasikia) Tuachane na mazungumzo haya ewe Ali.

**Ali:** Lakini kwa nini hukubali ukweli.

---

## UADILIFU WA MASAHAHA

---

**Wahaab:** Mimi sikuongea lakini nimeshituka, sasa niambie ni kwa nini mnawaaibisha baadhi ya maswahaba na mnawako-soa?

**Ali:** Kwanza – Sisi hatuko dhidi ya maswahaba bali sisi na wao tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Pili – sisi Shia tunapenda na tunatawalisha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na tunachukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; kila aliyetumikia Uislam na kuutetea pamoja na Mtume (s.a.w.w.) katika wakati wa shida na akadumu katika imani yake sisi tunapenda na tunampa heshima zote. Na kila aliyepetuka njia ya sawa na akafanya vitendo vilivyo nje ya Uislam haipasi kumpenda bali tunakuwa dhidi yake kwa ajili ya kuutakasa Uislam na hawa, lakini nakuuliza ewe Wahaab je, mnasema kuwa masahaba ni ma’asum?

**Wahaab:** Hapana, bali tunakiri na kukubali kuwa ni waadilifu bila ya kuwa ma’asum.

**Ali:** Je mmefanya utafiti kamili wa maisha yao mmoja mmoja ikathibiti kwenu kutokana na utafiti kuwa wao wote ni waadilifu?

**Wahab:** Kwa kweli hakuna utafiti kamili katika hili bali kuna baadhi ya vitendo vyema ambavyo walivifanya na wametetea Uislam katika mwanzo wake na baadhi yao wametajwa katika hadithi za Nabii na hivyo sisi tunawahesabu kuwa ni kati ya waadilifu.

**Ali:** Hivyo kunaweza pakapatikana makosa na madhambi kwao?

**Wahab:** Ndio bila ya shaka.

**Ali:** Yakipatikana madhambi kutoka kwao hawatakuwa waadilifu sivyo?

**Wahaab:** Lakini ni wapi yalitokea makosa kwao?

**Ali:** Muhimu nijibu swali langu.

**Wahab:** Ndio hawatakuwa waadilifu.

**Ali:** Na inasihhi kuwakosoa ..... na kama akikosolewa sahaba kwa kitendo kilichotokea kwake kukosoa huku hakuhesabiwi ni kutoka nje ya Uislam na wala sio ukafiri si ndivyo hivyo?

**Wahaab:** sahihi.

**Ali:** Hivyo sisi Shia tunawakosoa masahaba ambao wamefanya vitendo vibaya na wamefanya mambo hatari kwa Uislam na heshima yake kisha sisi hatukosoi masahaba wote bali baadhi yao kama hali ilivyo katika Qur’ani tukufu.

**Wahaab:** Kwanza, wapi Qur’ani imekosoa baadhi ya masahaba? Pili ni vitendo vipi hivyo ambavyo unajaribu kuwasingizia baadhi ya masahaba?

**Ali:** Mwenyezi Mungu anasema: **“Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na wale walioamini pamoja naye ni wakali kwa makafiri, ni wenye huruma baina yao utawaona ni wenye kurukuu na kusujudu wanataka fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu, alama zao..... Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini na kufanya mema kati yao maghfira na malipo makubwa.”**<sup>31</sup>

**Tazama ewe Wahaab:** neno - **kati yao** - yaani sio wote ambao walikuwa pamoja na Mtume (s.a.w.w.) ni waumini na ni wakali kwa

<sup>31</sup> Suratul- Fatiha: 29

makafiri, kwa maneno mengine sio kila sahaba anastahiki maghfira na malipo.

**Wahaab:** Ajabu sikugundua kubagua huku katika maisha yangu yote pamoja na kwamba mimi nimesoma Suratul-fatiha mara nyingi.

**Ali:** Amesema Mwenyezi Mungu: **“Hakuwa Muhammad isipokuwa ni Mtume walipita kabla yake Mitume wengi je akifa au akiuliwa mtarejea nyuma kwa visigino vyenu, atakayegeuka nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru Mwenyezi Mungu chochote; na Mwenyezi Mungu atawalipa wenye kushukuru.”**<sup>32</sup>

Aya hii imeeleza juu ya kugeuka na fitina ambayo itafuatia baada ya kuondoka Nabii (s.a.w.w.), katika nafasi ya ukhalifa na mengineyo na msemu huu (*inqalabtum alaa a’aqabi kum*) yaani baadhi ya watu walikuwa katika nafasi ya mwanzo lakini watageuka na hakuna shaka kwamba ni kati ya masahaba na wala sio wafuasi wa Musailamah au mabedui au wanafiki kwa sababu Aya inazungumza juu ya waumini, na Nabii (s.a.w.w.) ameunga mkono kwa Hadithi yake juu ya mapinduzi haya ambayo yatafuatia ambapo alisema: “Mimi nitawatangulia katika hodhi (birika), atakayelifikia atakunywa kwayo na hatapata kiu abadani, wataingia watu nawajua na wananjua kisha kutawekwa kizuizi baina yangu na yao, nitasema: hakika wao ni katika umma wangu, nitaambiwa: hakika wewe hujui waliyoyabadilisha baada yako, nitasema: maangamio maangamio kwa aliyebadilisha baada yangu.”<sup>33</sup>

**Wahab:** Lakini hujanitajia baadhi ya vitendo vyao viovu ambavyo tunaweza kuvikosoa, na vile vile nitajie katika rejea zetu za kisunni pamoja na kwamba naheshimu sana rejea zenu.

<sup>32</sup> Suratu Al- Imran: 144

<sup>33</sup> *Sahih Bukhariy*, Juz. 9, Uk. 57, *Sahih Muslim* Juz.7, Uk: 96 na *Musnad Ahmad* Juz. 5, Uk: 333 na mifano ya hadithi hizi katika *Bukhariy*, Juz. 8, Uk: 151

**Ali:** Sawa, nakutajia haya, Ama kuhusu Khalid bin Walid Mtume alishasema juu yake: “Ee Mwenyezi Mungu mimi niko mbali na aliyoyafanya Khalid.”<sup>34</sup> Haya ni katika uhai wa Nabii (s.a.w.w.). Ama baada ya kuondoka Nabii, Khalid alimua Malik bin Nuwaira kwa dhulma na akazini na mke wake, na Umar bin Khattab akamtaka Abu Bakr ampige haddi kwa kuuwa kwake na kuzini isipokuwa Abu Bakr alikataa na kujizuia.<sup>35</sup> Na kukataa huku ni kosa kwa Abu Bakr kwa sababu yeye hakutekeleza hukumu. Ama Aisha alikuwa anamlaani Uthmani bin Affan na kumkufurisha.<sup>36</sup> Ni juu yako kuuliza nafsi yako, ni ipi hali ya Athmani akikufurishwa na Aisha.

Ama Umar aliharamisha mambo yaliyokuwa halali wakati wa Nabii (s.a.w.w.) mfano muta’a ambayo alisema juu yake: “muta’a mbili zilizokuwepo wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu mimi naziharamisha,”<sup>37</sup> na Umar alimtuhumu Mughira bin Shu’uba kwa ufasiki na akamwambia wewe ni mtu fasiki.<sup>38</sup>

Ama Aisha alitoka wazi wazi dhidi ya Amirul-muuminina (a.s.), na vile vile Muawiya, Amru bin Aasi, Twalha na Zubeir. Ama Sa’ad bin Abi Waqaas alikataa kutoa bayi’a kwa Imamu Ali (a.s.) na alimuuwa Mar’awan bin Al-Hakam na Twalha bin Ubaidallah<sup>39</sup> katika vita ya Jamal, na wote walikuwa katika jeshi la Aisha na Umar aliyekuwa anataka Khalid auliwe, yeye hakumuwa aliposhika ukhalifa wa waislamu, na Uthman alimfukuza Abu Dharr na akampiga Abdallah Ibnu Mas’ud.

<sup>34</sup> *Tarakhul-Yaaqubiy* Jz: 2, uk:61 Fatuh Makka na *Tarikhu Twaabariy* Jz: 2 uk: 164

<sup>35</sup> Tazama kwa kisa hiki kwa kirefu zaidi katika *Tarikhu Twabariy* Jz: 2, uk: 273

<sup>36</sup> *Tarikhul-Yaaqubiy* Jz: 2, uk: 175 na uk:180

<sup>37</sup> *Alikaamul-Qur’ani* cha Jaswas Jz: 2, uk: 184

<sup>38</sup> *Tarakhul-yaaqubiy* Jz: 2, uk: 155

<sup>39</sup> *Tarikh ibn al-Wardi* J; 1 uk:149 chapa ya Darul-kutubl-ilimi, Beirut



**Wahaab:** Imetosha ewe Ali, yalikuwa wapi yote haya! Je, yapo kwetu?

**Ali:** Ndio na niliyokutajia ni machache kati ya rundo, nayo ni sehemu chache.

**Wahaab:** Lakini Ahlus-Sunna wanasema kuwa wao walifanya ijitihadi na wakakosea.

**Ali:** Vema sasa nijibu swali hili ili ujue maana ya neno hilo. Hakika Umar alikuwa anamtaka Abu Bakr amuuwe Khalid naye akakataa, na Umar alipochukua ukhalifa hakumuwa kwa nini? Kama anastahili kuuliwa kwa tuhuma hiyo? Kosa liko wapi na ijitihadi iko wapi? Katika mkanganyiko huu.

**Wahaab:** Sijui nisemeje.

**Ali:** Vivyo hivyo vitendo vingine vilivyobakia, je unaona kuna ijitihadi?

---

## MUTA'A

---

**Wahaab:** Umetaja katika mazungumzo yako muta'a vipi mnaihalalisha na Nabii (s.a.w.w.) alishaiharamisha?

**Ali:** Mimi nimekuambia kwamba Nabii hakuharamisha bali aliiharamisha Umar, na kauli ya Umar sio hoja kwa waislam kwa sababu yeye sio Nabii wala Imamu aliyewekwa na Mwenyezi Mungu bali ni mtu anakosea na kupatia bali hana haki ya kuharamisha aliyoyahalalisha Nabii wala kuhalalisha aliyoyaharamisha Nabii (s.a.w.w.).

**Wahaab:** Lakini sisi tunapokea kuwa Nabii aliharamisha.

**Ali:** Hapana hakika Qur'ani iliteremka na sheria ya muta'a katika kauli yake (s.w.t.): **“Ambao mmestarehe nao miongoni mwao wapeni mahari yao.”**<sup>40</sup> Watu wote wameafikiana kwamba makusudio yake ni ndoa ya muta'a yaani ya muda, na imepokewa kutoka kwa jamaa na kati yao ni Ibnu Abbas, Ibnu Mas'ud, Abdullah ibn Umar na Ubayya bin Ka'ab.<sup>41</sup> Ndio mmepokea kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ameiharamisha katika vita ya Khaibar tu kama ilivyo katika Bukhari na hii ina maana kwamba baada ya Khaibar hukumu ilirejea kuwa halali kama iliyokuwa, kwa ajili hiyo mmepokea yanayounga mkono hayo kwamba aliihalalisha siku ya Hijjatul-widaa.<sup>42</sup> Lakini kama utachunguza katika maneno ya Umar ungekuta kwamba ilikuwa halali kwa sababu yeye amesema: “Zilikuwa halali wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu,” hivyo ilikuwa halali wakati wa Nabii (s.a.w.w.).

Kisha sisi tunazo riwaya mutawatir na kongamano la Ulamaa wa Shia limesema juu ya riwaya za Ahlul-bait wa Nabii (s.a.w.w.)

<sup>40</sup> Suratun Nisaa: 23

<sup>41</sup> Anawawiy katika *Muslim* Juz. 9, Uk: 179

<sup>42</sup> *Sahihil Muslim* ; Kitabun-Nikah Juz. 4 Uk. 134

kwamba ni halali hadi siku ya Kiyama. Hata katika upande wa mtazamo wa kijamii muta'a inakuwa na faida sana ili zinaa na uasherati usienee. Kwa sababu hiyo anasema Al-Imam Ali (a.s.): "Kama si Umar kukataza muta'a asingezini isipokuwa muovu."<sup>43</sup>

---

<sup>43</sup> *Tafsiri Twabary* Jz: 5: uk. 13

---

## UKHALIFA

---

**Wahaab:** Mwisho na baada ya kunipa mwanga na kuniondolea pazia la giza na ujahili machoni mwangu, naomba unitajie dalili ambayo mnaitumia juu ya kwamba Amirul-muuminina Ali (a.s.) ni khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wasii wake baada yake bila ya kutenganisha.

**Ali:** Ama tuitakidi kuwa Nabii alifariki bila ya kumuusia yeyote au tuitakidi kwamba Nabii (saww) aliusia kabla ya kifo chake. Ama ya kwanza: inakhalifu akili, hali halisi na mwendo wa manabii, kwa sababu wenye akili wamekubali jambo la kutoa wasia ndio maana tunapata wasia tangu zamani bali tunakuta wasia hata katika watu wasio kuwa na dini, na vitabu vya sira na tarikh vimejaa wasia wa manabii kwa mawasii wao ambao wanawafuatia kwa sababu unaunganisha yaliyopita na yaliyopo na kupanga hali halisi ya wanadamu. Vipi tuseme kuwa Nabii (s.a.w.w.) hakuusia kwa yeyote pamoja na kwamba wasia ni katika Sunna za Mitume:

**“Na Ibrahim aliusia wanawe na Ya’aqub....”<sup>44</sup>**

Na inafahamika kwamba Nabii (s.a.w.w.) sio wa mwanzo kati ya mitume bali ni bwana wao na mbora wao hadi, hapa nimefikia pamoja nawe ewe Wahaab kwenye ulazima wa kusema kwamba Nabii (s.a.w.w.) aliusia kulingana na sira ya mwenye akili, Manabii na Qur’ani ambayo imeamuru kuusia na sisi tuko mbele ya mambo mawili:-

1. Ama Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alijali mustakbali wa umma wake na jamii yake.
2. Na ama asiyekuwa yeye aliujali zaidi kuliko yeye, mfano khalifa wa kwanza na wa pili ambapo mmoja wao alimuusia mwingine.

---

<sup>44</sup> Suratu baqara: 132

Na jambo la pili ni batili kwa hali halisi na kwa kauli yake (s.w.t.) **“Yanamhuzunisha yanayokutaabisheni anakuhangai-kieni, kwa waumini ni mpole mwenye huruma.”**<sup>45</sup> Hivyo yeye anaujali zaidi kuliko Abu Bakr na Umar na ni wajibu awe ameusia kwa sababu ndiye mwenye majukumu makubwa zaidi – nakusudia kuwa dini ya Kiislam ni dini ya ulimwengu. vipi –ataiacha hivi hivi, haya yote ni dalili ya kimazingira na kiakili ewe Wahaab. Ama dalili za Sunna ni nyingi kati ya hizo ni:- Kauli yake (s.a.w.w.) kwa Ali: “Huyu ni ndugu yangu na khalifa wangu kwenu. ....”<sup>46</sup> na kauli yake (s.a.w.w.): “Huyu ni Ali bin Abu Twalib wasii wa Mtume wa Mola wa Walimwengu na Imamu wa wachamungu na kiongozi wa Ghurul- Muhajaliyna (waumini ).<sup>47</sup>

Na kutoka kwa Anas bin Malik amesema: “Tulimwambia Salman muulize Nabii ni nani wasii wake?” Salmani akamwambia: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni nani wasii wako?” Akasema: “Ewe Salman, ni nani wasii wa Musa?” Akasema: “Yu’usha bin Nun.”

Akasema (s.a.w.w.): “Wasii wangu na mrithi wangu atakayelipa deni langu na kutimiza ahadi yangu ni Ali bin Abu Twalib.”<sup>48</sup> Na nyinginezo nyingi kati ya hadithi.

**Wahaab:** Umebarikiwa ewe Ali, na kushukuru kwa muongozo wako na kunipa mwanga.

**Ali:** Na mimi ninakushukuru pia ewe Wahab kwa roho nzuri ambayo inataka kujua kheri.

<sup>45</sup> Surat Tauba: 128

<sup>46</sup> *Tafsirul-Khazin* Jz: 3, uk: 372 chapa ya Darul- Maarifah-Beirut na *Kifayatul-Twalib*, babu 15

<sup>47</sup> *Tarikhul Baghdad* Jz: 11, uk:,112 chapa ya As-Sa’adah-Misri.

<sup>48</sup> *Riyadhur-Nadhar* ya Twalib Jz :2, uk. 279 na *Fadhail-sahaba* cha Ahmad Jz: 2, uk: 10. Hadithi namba:1052.

---

---

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA**

---

### **AL-ITRAH FOUNDATION**

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana

39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata



60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)

81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi

103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqaalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono

168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye

189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msugvano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii

210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Mjadala wa Kiitikadi



---

---

**KOPI NNE ZIFUATAZO  
ZIMETAFSIRIWA  
KWA LUGHA KINYARWANDA**

---

1. Amateka Na Aba’Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n’amavuko by’ubushiya
4. Shiya na Hadithi

---

---

**ORODHA YA VITABU VILIVYO  
CHAPISHWA NA  
AL-ITRAH FOUNDATION KWA  
LUGHA YA KIFARANSI**

---

1. Livre Islamique